

USIMAMIZI WA KARADHA KISHERIA TANZANIA

1. UTANGULIZI

Usimamizi wa karadha hapa Tanzania hutegemea zaidi mikataba, muhtasari wa kesi za karadha pamoja na sheria nyingine zinazohusu karadha. Sheria hizo ni pamoja na sheria ya mikataba ya tort na kutoa miliki.

Karadha ya fedha inahusisha mali binafsi na vipengele vya sheria mikataba, na fedha. Hapa Tanzania, vipengele vya kusimamia karadha viko kwenye sheria tofauti. Sheria hizo ni zile zinazosimamia mauzo, mikataba na mabenki na taasisi za fedha. Sheria nyingine zinazohusu karadha ni pamoja na usajili wa mali, mikataba inayotoa mvuto kwenye mali na zile zinazosimamia haki za wadau kwenye mali husika.

Mfumo uliopo wa kisheria haukidhi mahitaji ya karadha hapa Tanzania. Aidha, sheria hizi hazishabihiani kuwezesha karadha kuendelea. Sheria za jumuiya ya madola hazijakamilika kuwezesha kutumika kwa ajili ya karadha na siyo lazima zitumike hapa Tanzania.

Mifano ya mapungufu ya sheria hizo ni pamoja na:-

- Hakuna tofauti inayokubalika kisheria baina ya karadha na ununuzi wa mali kwa mkopo. Sheria ya mauzo kwa mkopo haiwezi kukidhi mahitaji ya karadha.
- Ni vigumu kwa mkopeshaji kupokonya mali kisheria kwa kutumia mfumo wa mahakama ambao huchukua muda mrefu na una urasimu mkubwa pale mkopaji anaposhindwa kulipia karadha.
- Mfumo wa sheria kwa sasa unazuia usimamizi wa karadha.
- Mbali na sheria ya kodi, sheria nyinginezo hazibainishi karadha kwa ajili ya kudai fidia mahakamani.
- Mfumo wa kisheria haubainishi haki na majukumu ya wadau wote kwenye karadha, hasa zile zinazohusu wadau watatu.

Utafiti uliofanywa na IFC umebaini kuwa hakuna sheria inayosimamia karadha hapa Tanzania. Pia hakuna kesi zinazohusu karadha kwa kukosekana huduma ya karadha na mahakama hazijapata fursa ya kushughulikia kesi za karadha.

2. SHERIA ZENYE KUSHUGHULIKIA KARADHA

Sheria zifuatazo zina vipengele vyenye kuhusika na karadha:

- Sheria ya Mikataba - 1961

- Sheria ya Mauzo
- Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha - 2006
- Sheria ya Makampuni - 1931
- Sheria ya Usalama Barabarani - 1973
- Sheria ya Ufilisi - 1930
- Civil Procedure Code - 1966
- Chattels Transfer 1931
- Sheria za Kodi (ongezeko la thamani , forodha, ushuru wa stempu na Mapato)

Vile vile sheria ya jumuiya ya madola udhamini, tort, mkataba na kuhamisha miliki zinashughulika karadha.

Sheria zilizotajwa hapo juu zinabainisha yafuatayo:

3. MIKATABA YA KARADHA KAMA MIKATABA YA UDHAMINI

Karadha ya fedha ni mkataba baina ya mkopeshaji na mkopaji. Karadha husimamiwa na sheria ya mikataba. Kipengele namba 8 cha sheria hii kinahusu ukomo wa madai baina ya wadau wanaohusika na mkataba huo. Karadha kama mauzo kwa mkopo, ina masharti kama yalivyo kwenye sheria. Mkataba na wajibu anayetoa udhamini na anayedhaminiwa. Kwenye karadha ya fedha, mkopeshaji ni mdhamini na mkopaji ni mdhaminiwa.

Sheria hii ya udhamini inabainisha majukumu ya mkopeshaji kwa mkopaji itokanayo na mali iliyokopeshwa, na haidhuru kama mdhamini alikuwa anajua kuwa anao wajibu huo au la. Vipengele vya sheria vilivyoko kwenye sheria ya mikataba havitoshelezi mahitaji ya karadha.

Nchi za Uingereza na India zimeandaa misingi ya kusimamia udhamini kwenye sheria ya mikataba. Hata hivyo misingi hii haitambuliki kwenye mahakama za Tanzania.

Kwenye karadha ya fedha, mdhamini kawaida ni mkopeshaji (ambayo ni taasisi ya fedha). Changamoto iliyopo ni kuandaa misingi ya udhamini kwenye sheria ya karadha inayotoa ukomo wa madai kwenye karadha na kiasi cha ukomo huo kwa mkopeshaji.

4. MADAI KWA KUTUMIA MALI ILIYO KWENYE KARADHA

Ingawa kwenye karadha ya fedha mkopeshaji anabaki kuwa mmiliki wa mali iliyo kwenye karadha, mkopeshaji hatakiwi kuwa na wajibu wa ubora wa mali hiyo. Mkopeshaji kwa kawaida ni taasisi ya fedha ambayo haihusiki na kuchagua mali inayowekwa kwenye karadha, na hivyo hawezi kudhamini ubora wa mali hiyo. Endapo udhamini utatambuliwa kisheria, udhamini huo utatakiwa kutoka kwa wauzaji, na sio kwa mkopeshaji.

Uzoefu wa karadha za fedha popote duniani umeonyesha kuwa mkopeshaji hausiki na madai yahasuyo ubora wa mali iliyo kwenye karadha. Wauzaji kwa kawaida huarifiwa kuwa watawajibika kwa ubora wa mali zilizo kwenye karadha pale ambapo mali husika huwekwa kwenye karadha. Kuna haja ya kuwa na misingi itakayobainisha jukumu la muuzaji kudhamini mali iliyo kwenye karadha.

Sheria ya mauzo kwa mkopo huweka bayana majukumu ya udhamini kwa mkopeshaji kuhusu ubora wa mali husika.

5. USIMAMIZI WA KARADHA

Karadha itafanikiwa iwapo mkopeshaji atakuwa na uwezo wa kusimamia karadha, kupokonya mali iliyo kwenye karadha endapo mkopaji atashindwa kulipia karadha.

Urahisi wa usimamizi, makubaliano kwenye karadha na hatua za kisheria zisizochukua muda mrefu ni muhimu pia kwenye karadha. Urahisi wa kupokonya mali iliyo kwenye karadha, na kutokuwepo urasimu kwenye mahakama pia husaidia karadha kufanikiwa.

Uzoefu wa mahakama hapa Tanzania umeonyesha kuwa kesi za madai zinachukua muda mrefu. Wakopaji pia huutumia mfumo huu wa mahakama kulinda maslahi yao kwa kuweka pingamizi la mahakama linalomzuia mkopeshaji kupokonya mali iliyo kwenye karadha. Sheria ya madai ina kipengele cha kuharakisha uamuzi wa mahakama kuhusu madeni. Hata hivyo, kipengele hiki hakihusishi madeni ya karadha, na uzoefu umeonyesha kuwa madai haya yamekuwa yakichukua muda mrefu.

Ili karadha iendelee, kuna haja ya sheria kuwa wazi kuhusu ukusanyaji wa madeni ya karadha kufanyika kwa muda mfupi iwezekanavyo.

6. KARADHA KAMA BIASHARA YA BENKI

Karadha hapa Tanzania inafanywa na mabenki. Utafiti uliofanyika ulibainisha kuwepo kwa taasisi binafsi kadhaa za fedha zinazojishughlisha na karadha. Makampuni hayo hayajaanza shughuli za karadha. Mabenki na taasisi za fedha husimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa sheria ya mabenki na taasisi za fedha. Sheria hii inatambua mabenki kuwa ni pamoja na karadha ya fedha. Wadau kadhaa wanaamini kuwa karadha inatakiwa kutambulika kama mojawapo ya biashara za mabenki.

Hata hivyo, mabenki yanazuiwa kuifanya biashara ya karadha kwa mujibu wa kanuni za mikopo za mabenki za 2001 ambazo zinatoa kiwango cha juu cha 50% cha mtaji wa benki.

7. MADAI YA WADAU WA TATU KUTOKANA NA MALI ZILIZO KWENYE KARADHA

Madai baina ya mkopaji na mkopeshaji yatokanayo na mali iliyo kwenye karadha husimamiwa na mkataba wa karadha.

Sheria ya mikataba, pia inatoa maelekezo yanayosimamia madai baina ya wakopeshaji na wakopaji chini ya sheria ya udhamini. Kwa mujibu wa sheria ya jumuiya ya madola, mkopeshaji anaweza kuwajibika kwa mdau wa tatu kudhurika na matumizi ya mali iliyo kwenye karadha endapo mkopeshaji ataonekana kutokuwa mwangalifu kwa wadau hawa. Hakuna mwongozo wa kutosha kuhusiana na madai ya aina hii.

Uzoefu umeonyesha kuwa mkopeshaji humtaarifu mkopaji kutumia mali iliyo kwenye karadha kwa usalama, kuitunza na kuwa na bima yenye kukinga wadau wengine zaidi ya mkopeshaji na mkopaji.

Mfumo wa sheria wa karadha utatakiwa kutoa mwongozo wa kutosha kuhusu madai ya wadau wa tatu pamoja na mazingira ya mkopeshaji kutodaiwa.

8. UANDIKISHAJI WA MALI ILIYO KWENYE KARADHA NA MIKATABA

Uandikishaji wa mali kisheria hupendelewa na mkopeshaji kwa sababu mbalimbali, ikiwemo mkopeshaji kuandikisha mvuto wake kwenye mali husika ambayo kuandikisha mali hii hutumika kama taarifa ya kisheria kwa wadau wa tatu kuwa umiliki wa mali husika hauwezi kuhamishwa kisheria.

Hapa Tanzania, sheria ya uhamishaji wa umiliki – 1931 huwezesha uandikishaji wa umiliki wa mali. Karadha pia inaweza kuandikishwa chini ya sheria hii.

Karadha ikishaandikishwa, wahusika wengine wowote wanategemewa kuwa wanafahamu karadha hiyo na masharti yake yote.

Uandikishaji wa karadha huhusisha mikataba tu, na siyo mali iliyo kwenye karadha. Kutokana na hilo, hakuna haja yakuthibitisha mali husika.

Hapa Tanzania kuna rejista ya magari, lakini mali nyingine zinazohamishika ambazo zinaweza kuwa kwenye karadha hazina rejista. IFC haipendekezi kuanzishwa kwa usajili wa mali ili karadha iweze kuendelea.

9.5. TOFAUTI YA KARADHA YA FEDHA NA MAUZO KWA MKOPO

Mauzo kwa mkopo yanafanana kwa karibu sana na karadha ya fedha.

Wakati ambapo mkopaji kwenye mauzo kwa mkopo anayo fursa ya kusitisha malipo na kurudisha mali kwenye mkataba, mauzo kwa mkopo yanatofautina na karadha ya fedha kwa sababu uchakavu wa mali hurudishwa kwa mkopeshaji mauzo ya mkopo. Mkataba

ukisitishwa, mwenye mali hurudishiwa mali iliyo na thamani pungufu kuliko malipo ya mali mwishoni mwa mkataba. Kwenye karadha ya fedha, mkopeshaji anayo nafasi ya kurejesha thamani ya mali kwa kupokea malipo ya ununuzi wa mali au fidia endapo mkataba utasitishwa.

Kwenye karadha ya fedha, umiliki wa kisheria wa mali iliyo kwenye karadha unabaki mikononi mwa mkopeshaji kwa kipidi chote cha karadha hadi malipo ya mwisho ya karadha yakishalipwa na mkopaji akishaamua kuinunua mali iliyo kwenye karadha. Kutokana na mikataba ya karadha, haitegemewi kuwa upokonyaji wa mali iliyo kwenye karadha utakuwa na ugumu wowote, bali utahitaji amri ya mahakama kuruhusu upokonyaji.

10. MAUZO YA MKOPO HAPA TANZANIA

Sheria ya mauzo ya mkopo hapa Tanzania inabainisha kuwa thamani inayohusika ni fedha za K Tanzania 60,000/= . Sheria inatoa haki kwa mkopeshaji kusitisha mkataba wakati wowote, na endapo mkopaji atakuwa ameshalipa $\frac{2}{3}$ ya bei, sheria inamtaka mkopeshaji kuomba hati ya mahakama kupokonya mali iliyo kwenye mauzo ya mkopo.

Sheria hii ambayo ilitungwa wakati wa uchumi hodhi, inatoa majukumu makubwa kwa wamiliki wa mali.

Hapa Tanzania, sheria ya mauzo kwa mkopo hutoa kinga kwa watumiaji wa bidhaa ndogo ndogo, kinga ambayo inaaminika kuwa ni muhimu kwa watumiaji wa kisheria.

Kwenye nchi nyingi za jumuiya ya madola, mauzo kwa mkopo ni njia mojawapo ya kumiliki mali, hasa hizi ndogondogo, ambayo huzuia upokonyaji wa mali iliyozwa kwa mkopo. Nchini Uingereza, endapo mkopaji atakuwa ameshalipa $\frac{1}{3}$ ya bei ya mali iliyozwa kwa mkopo, sheria humtaka mkopeshaji kupata kibali cha mahakama kupokonya mali husika. Nia ya amri ya mahakama inatokana na ukweli kuwa mkopaji anapata huduma itokanayo na matumizi ya mali ya mkopo.

11. MAPENDEKEZO YA SHEIRA YA KARADHA

Kulingana na utafiti uliofanyika, IFC inapendekeza kuwepo kwa mfumo wa kisheria utakaosimamia karadha hapa Tanzania. Usimamizi huu utawezesha kuendelea kwa karadha.

Mfumo wa sheria unapendekeza kulenga yafuatayo:

- Kutofautisha karadha na njia nyingine zozote za kumiliki mali bila ya kuzilipia kwanza.
- Kuanzisha njia rahisi za kusimamia karadha.

- Kubainisha haki na majukumu ya wadau wote wa karadha na hasa pale ambapo karadha itahusisha wadau watatu.
- Kuondoa mgongano uliopo kwenye sheria zilizopo ambao unazuia kuendelea kwa karadha.
- Kutoa fursa ya kuandikisha karadha na mali zilizo kwenye karadha.
- Kutoa mwongozo kuhusu madai ya mdau wa tatu yatokanayo na matumizi ya mali iliyo kwenye karadha.
- Kubainisha taasisi zinazoweza kushiriki kwenye karadha.

Mfumo wa kisheria wa karadha unaweza kuwepo kwa kuanzisha sheria ya karadha au kuzifanyia marekebisho sheria zilizopo. Bila kutegemea sheria mpya au kurekebisha sheria zilizopo, mfumo wa kisheria wa karadha hapa Tanzania utahitaji kuoanisha sheria zote zilizopo pamoja na sheria za jumuiya ya madola na utatakiwa kutoa uhuru wa kutosha kwa wadau wa karadha kuingia kwenye mikataba ya karadha.

12. KANUNI NA USIMAMIZI WA KARADHA

Karadha ya fedha huhusisha masoko ya fedha, na hivyo itahitaji usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania. Usimamizi wa karadha unaweza kufanywa kwa kusimamia mabanki na Taasisi za fedha zenye kuhusika na karadha, au kuwa na taasisi zisizo za fedha zilizoandikishwa kama makampuni ya karadha.

Benki na Makampuni ya Karadha	Taasisi za Karadha zisizokuwa za fedha
<p>Benki Kuu ya Tanzania husimamia mabanki na Taasisi za fedha.</p> <p>Utaratibu wa kimataifa wa usimamizi wa karadha umeonyesha kuwa karadha pia husimamiwa na benki kuu kwa kuwa taasisi hizi hupokea amana kutoka kwa umma. Kampuni tanzu za mabanki zenye kujihusisha na karadha zitatakiwa kusimamiwa na Benki Kuu.</p>	<p>Uzoefu umeonyesha kuwa karadha haisimamiwi na Benki Kuu kwa taasisi hizi ambazo hazipokei amana toka kwa umma. Hata hivyo, jukumu la benki kuu kama msimamizi wa mikopo na sera za fedha itaiweka benki kuu kuwa msimamizi wa karadha zinazotekelezwa na taasisi zisizopokea amana za umma kwa sababu karadha inahusisha masoko ya fedha.</p> <p>Hivyo, usimamizi wa Benki Kuu utatakiwa, japo kwa kiwango kidogo.</p>

13. MFUMO WA KODI KWENYE KARADHA

Mfumo wa kodi kwenye karadha unaguswa na sheria mbali mbali za kodi kama inavyoelezwa hapa chini:

14. KODI YA MAPATO (NAFUU YA KODI)

Sheria ya kodi ya mapato ya 2004 imeanzisha mapendekezo mapya kwenye karadha. Karadha ya fedha itazingatia mwenye kunufaika na matumizi ya mali zaidi ya umiliki wa kisheria. Mabadiliko haya yataleta urahisi wa utekelezaji wa sheria hii na pia kuioanisha na jinsi ya kutumia karadha hii kiuhasibu kufanana na tafsiri ya kodi. Nafuu hii pia itatambua ukweli kuwa mtumiaji ndiye anayefaidika na nafuu ya kodi kutokana na matumizi yake na sio kutokana na umiliki.

Sheria hii inatambua karadha ya fedha kuwa:

- Mkataba unaobainisha kuhama miliki ya mali mwishoni mwa mkataba;
- Mkopaji anayo fursa ya kununua mali baada ya mkataba, kwa bei iliyokubalika kabla ya kuingia kwenye mkataba wa karadha;
- Muda wa karadha unazidi asilimia 75 ya matumizi ya mali iliyo kwenye karadha;
- Thamani ya mali iliyo kwenye karadha ni chini ya asilimia 20 ya thamani ya mali mwanzoni mwa karadha;
- Iwapo karadha imeanza kabla ya asilimia 25 ya muda wa matumizi yake, thamani ya sasa ya mali, ukitoa malipo ya karadha ni sawa au zaidi ya asilimia 90 ya thamani ya mali mwanzoni mwa karadha au;
- Mali iliyo kwenye karadha ni maalum kwa matumizi ya mkopaji na mwishoni mwa karadha, mali hiyo haitatumiwa tena na mdau yeyote mwingine.

Matumizi ya maelezo hayo hapo juu:

- Kodi ya mapato kuhusu malipo ya karadha yatawiana na matumizi ya mali kuliko umiliki wa mali kisheria.
- Wakopeshaji watachukuliwa kuwa wamehamisha miliki kwenda kwa wakopaji ili wakopaji wapate nafuu ya kodi.
- Malipo ya karadha yatachukuliwa kama riba iliyolipwa na mkopaji na marejesho ya mkopo. Riba tu ndiyo itakayopata nafuu ya kodi.

- Mali zitakazohusika ni zile za kudumu na kushikika na zisizoshikika, hivyo nafuu ya kodi itakuwa kwa mali zote hizi.
- Mfumo wa kodi utatambua viwango vya uhasibu vya kimataifa vihusavyo karadha yaani IAS 17.
- Malipo anayopokea mkopeshaji, atayahusisha mapato ya riba na marejesho ya mkopo ambao ni thamani ya mali iliyo kwenye karadha.

Kumekuwa na mawazo tofauti ya nani apate nafuu ya kodi kati ya mkopeshaji na mkopaji. Wengine wanadhani mkopeshaji anastahili kufidia uwekezaji wake, ambapo wengine wanadhani mkopaji ndiye anayestahili.

15. THAMANI YA ONGEZECO LA THAMANI (VAT)

Kodi ya ongezeko la thamani haitofautishi malipo ya karadha, na yote yanatozwa kodi. Kodi hii inaota upendeleo kwa riba za mikopo ya kawaida ambazo hazilipiwi kodi ya ongezeko la thamani.

Karadha ya fedha ni njia mojawapo ya kulipia mali. Kodi ya ongezeko la thamani haitambui karadha hii kama njia ya malipo. Tafsiri ya kodi ya ongezeko la thamani ni kuwa karadha ni sawa na mauzo ya mali nyinginezo ambazo zinatozwa kodi hii. Kwa upande mwingine, mikopo haitozwi kodi hii, hivyo kodi ya ongezeko la thamani hutoa upendeleo kwa mikopo. Hakuna tofauti ya karadha na mikopo iliyo wazi kwenye sheria hii.

Sheria hii humtaka mkopaji kulipa kodi ya ongezeko la thamani anaponunua mali na pia wakati wote wa malipo ya karadha. Mkopaji atakaponunua mali mwishoni mwa karadha atatakiwa kuulipia kodi ya ongezeko la thamani tena. *Endapo tofauti ingetolewa, mkopaji asingelipa VAT mara zote hizi.*

Wakati ambapo karadha ina kodi hii, sio wakopaji wote wenye fursa ya kudai marejesho ya kodi la ongezeko la thamani kwa sababu hawajaandikishwa kwa kuwa na kiwango cha mauzo chini ya kiwango kinachotakiwa kuandikishwa. Washiriki wengi pia ni makampuni madogo madogo na ya kati na ambayo yamesamehewa kama vile mabanki na taasisi za fedha.

Ikiwa muuzaji atashirikisha benki, muuzaji atatakiwa kudai kodi ya ongezeko la thamani kwenye mali iliyozwa kwa benki na kodi ya ongezeko la thamani iliyotolewa itarejeshwa kwa benki au mkopeshaji.

Kwa vile mali iliyozwa inahusisha mali na mkopo uliotolewa na benki kwa mkopaji, benki (ambayo imesamehewa) itahesabu kuwa kodi ya ongezeko la thamani iliyolipwa ni sehemu ya kodi iliyolipwa kwa ununuzi na mkopaji na itatumia njia mojawapo ya msamaha kudai marejesho ya VAT.

16. KANUNI KUU ZA KODI YA ONGEZECO LA THAMANI KWA BENKI

- Karadha zote isipokuwa za ardhi na majengo ya kuishi zinatakiwa kulipiwa kodi ya ongezeko la thamani.
- Karadha ya uendeshaji hutambulika kama mauzo ya huduma na hivyo hulipiwa kodi ya ongezeko la thamani. kila malipo yanapopokelewa na mkopeshaji kwa kiwango cha asilimia 20.
- Mkopaji atatakiwa kukokotoa kama kodi ya kodi ya ongezeko la thamani. manunuzi yote ya mali toka nje ya nchi isipokuwa mali za kudumu kama mtaji ambao umesamehewa kodi ya ongezeko la thamani.
- Malipo yote ya nje hayana kodi ya ongezeko la thamani. Manunuzi ya mali kwa ajili ya mashirika ya dini na mahospitali pia yamesamehewa kodi ya ongezeko la thamani.
- Kodi ya ongezeko la thamani inaonekana kuwa ni moja ya kikwazo kikuu cha kukua kwa karadha hapa Tanzania.

Utafiti wa IFC ulibainisha kuwa:

- Kodi ya ongezeko la thamani haijatofautisha karadha hivyo kutozwaji wake sio bayana. Kama tofauti ya karadha ingekuwapo, utozwaji wake ungekuwa tofauti. Kwenye karadha ya uendeshaji; kodi ya ongezeko la thamani hulipwa na mkopeshaji wakati wa ununuzi na hutozwa mkopaji kila malipo ya karadha yanapofanyika.
- Marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani kwa mabenki; sheria imetoa njia mbili za kudai marejesho kwa mabenki yahasikayo na karadha. Njia hizi hazina kivutio kwa mabenki kushiriki kwenye karadha kwa sababu mabenki haya hayawezi kurejeshewa kodi ya ongezeko la thamani iliyolipwa kwenye karadha.
- Makampuni yasiyoweza kupunguza malipo ya kodi ya ongezeko la thamani wakati yanapotoa huduma zao yanaona karadha kuwa ni ghali na isiyo na manufaa kwao. Makampuni mengi ya uhandisi yanapewa kazi na makampuni ambayo hayana kodi ya ongezeko la thamani na hivyo kukosa namna ya kurejeshewa kodi ya ongezeko la thamani. iliyolipwa.

Ikiwa kodi ya ongezeko la thamani itatozwa kwenye karadha na wakopeshaji; basi itaongeza gharama ya vifaa vinavyokopeshwa kwa asilimia 20 kwa makampuni yasiyoweza kurejeshwa malipo ya VAT.

- (a) Tofauti na mikopo ya kawaida, karadha hulipiwa kodi ya ongezeko la thamani. Kodi hii inaifanya karadha kuwa ghali kuliko mikopo ya

kawaida. Kodi ya ongezeko la thamani kwa biashara ndogo ambazo hazijasajiliwa kutoza kodi ya ongezeko la thamani au zinazoshugulika na bidhaa ambazo hazitozwi VAT itaifanya karadha kuwa ghali kuliko mikopo ya kawaida kwa sababu wakopaji hawa hawataweza kudai marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani. Iliyolipwa kwenye karadha.

IFC haipendekezi kufutwa VAT kwenye karadha, bali iweze kurejeshwa kwa walipaji. Iwapo kodi ya ongezeko la thamani itatozwa kwenye mauzo, kuhamisha miliki ya mali iliyo kwenye karadha kutatozwa kodi ya ongezeko la thamani pia.

- (b) Serikali ifikirie nafuu ya kodi kwa biashara ndogo zisizosajiliwa kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani kwenye karadha. Mabenki yenye kujihusisha na karadha yanapendekeza kuwa kodi ya ongezeko la thamani litathminiwe tofauti miongoni mwa huduma za benki na karadha.
- (c) Sheria ya kodi ya ongezeko la thamani inahitaji marekebisho ilikuweka bayana tofauti ya karadha ya fedha na uendeshaji na vigezo vinavyotofautisha karadha hizi kwa ajili yakutathmini kodi ya kodi ya ongezeko la thamani.
- (d) Kuna haja ya kuonisha mfumo wa kodi kwa nchi zote za Afrika Mashariki zinazohusu karadha. Mfumo wa kodi nchini Kenya hautambua nafuu ya kodi kwa wakopeshaji kwenye karadha na Uganda inajitahidi kufananisha mfumo wake na ule wa kodi ya Kenya. Tanzania imerekebisha mfumo wake wa kodi ili ufanane na Uganda. Mfumo wa kodi unaofanana utaweka fursa sawa kwa wadau wa karadha hapa Afrika Mashariki.
- (e) Kuna haja ya kutoa elimu kwa umma kwa wadau wote kuhusu faida za karadha hasa kwa biashara ndogo. Elimu hii itazingatia zaidi kubadilisha mtazamo wa wadau kuhusu mikopo ikiwa ni pamoja na karadha, kujenga uelewa wao na nia ya kushiriki kwenye karadha. Elimu kwa umma ni pamoja na vyama vya kitaalamu, mabenki, biashara mbalimbali, mamlaka ya mapato na mahakama.